DCB COMMERCIAL BANK



Benki Kidijitali.
Bila Makato.
Bila Mipaka.

# MKUTANO MKUU WA 24 WA MWAKA

## NA TAARIFA YA BENKI KWA MWAKA 2025



# Benki Kidijitali.
# Bila Makato.
# Bila Mipaka.

Kaulimbiu hii inaakisi mwelekeo wa kimkakati wa benki ya DCB katika kuendeleza mageuzi ya kidijitali, kuimarisha ujumuishi wa kifedha na kutoa thamani endelevu kwa wanahisa, wateja, jamii na wadau mbalimbali.

**"Benki Kidijitali. Bila Makato. Bila Mipaka."** si kaulimbiu tu; ni ahadi ya DCB ya kurahisisha huduma za kibenki, kupunguza gharama na kuwawezesha wateja wetu kufikia mafanikio yao kupitia huduma zinazoendeshwa na teknolojia.



# YALIYOMO


05
TAARIFA ZA KAMPUNI

06
VIFUPISHO

07
**24.2** TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA ISHIRINI NA NNE WA MWAKA

08-12
**24.3** KUTHIBITISHA KUMBUKUMBU ZA MKUTANO MKUU WA 23 MWAKA ULIOFANYIKA TAREHE 19 JULAI 2025

13
**24.4** KUPOKEA NA KURIDHIA UTEKELEZAJI WA YATOKANAYO NA MKUTANO MKUU WA 23 WA MWAKA

14-22
**24.5** KUPOKEA NA KURIDHIA TAARIFA YA WAKURUGENZI WA BODI

23
**24.6** KUPOKEA TAARIFA YA KUISHA KWA MUDA WA WAJUMBE WA BODI YA WAKU-RUGENZI

24 - 25
**24.7** UCHAGUZI WA WAJUMBE WA BODI YA WAKURUGENZI

26
**24.8** KUPOKEA NA KUIDHINISHA UTEUZI WA MKAGUZI HURU WA HESABU KWA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 31 DISEMBA 2026

26
**24.9** KUPOKEA NA KURIDHIA PENDEKEZO LA MALIPO YA ADA KWA WAJUMBE WA BODI

26
**24.10** KUPANGA TAREHE YA MKUTANO MKUU WA 25 WA MWAKA

27-38
KIAMBATANISHO NA. 1

39 - 42
KIAMBATANISHO NA. 2




## TAARIFA ZA KAMPUNI



### OFISI ILIYOSAJILIWA

Jengo la DCB House Kitalu Na. 182 - R Magomeni Mwembechai,
S.L.P 19798
Dar es Salaam

### KATIBU WA KAMPUNI

Ms Regina Mduma
Jengo la DCB House
Kitalu Na. 182 – R
Magomeni Mwembechai
S.L.P 19798
Dar es Salaam

### WAKAGUZI

KPMG
The Luminary
2nd Floor, Haile Selassie Road, Masaki
S.L.P 1160
Dar es Salaam

### WANASHERIA

Excellent Attorneys
5th Floor Citi Plaza Building
Jamhuri Street
Dar es Salaam

Frostee Attorneys
4th Floor, Co- Architecture II Building Bridge India Street
S.L.P 70950
Dar es Salaam

Lawfront Advocates
S.L.P 31312
Mikocheni A, Garden Road
Dar es Salaam

Apex Attorneys Advocates
1st Floor, Scouts Building
Malik Road, Upanga
S.L.P 34674
Dar es Salaam

## VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| AGM | Mkutano Mkuu wa Mwaka |
| ATM | Mashine ya kutoa na kuweka fedha |
| ALCO | Kamati ya Mali na Dhima |
| BOT | Benki Kuu ya Tanzania |
| CIR | Uwiano wa mapato na matumizi |
| CMSA | Mamlaka ya masoko ya mitaji na dhamana |
| DCB | Benki ya biashara ya DCB |
| DSE | Soko la Hisa la Dar-es-Salaam |
| EAD | Kadirio la hasara ya mikopo isiyolipika ya benki |
| ECL | Matarajio ya baadaye ya hasara ya mikopo |
| EPS | Mapato kwa kila hisa |
| IASB | Bodi ya Viwango ya Uhasibu ya Kimataifa |
| IESBA | Bodi ya Viwango ya Maadili ya Kimataifa ya Wahasibu |
| IFRS | Viwango vya Kimataifa vya Taarifa za Fedha |
| LC | Barua za mikopo |
| LDR | Mkopo kwa uwiano wa amana |
| LGD | Hasara itokanayo na mkopo usiolipika |
| NPL | Mikopo chechefu |
| POCI | Mali zinazotarajiwa kuingiza hasara |
| ROUA | Haki ya matumizi ya mali |
| SGL | Ukopaji wa vikundi |
| SICR | Ongezeko Kubwa la hatari ya mikopo |
| SME | Wafanyabiashara wadogo na kati |
| SMR | Kiwango cha chini cha amana cha kisheria |
| SPPI | Malipo ya kianzio na riba |
| SPV | Kampuni ya makusudio maalum |
| TMRC | Taasisi ya Mikopo ya Nyumba ya Tanzania |
| TZS | Shilingi ya Kitanzania |
| USD | Dola ya Marekani |



Benki Kidijitali. Bila Makato. Bila Mipaka.

## 24.2 TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA ISHIRINI NA NNE WA MWAKA

Taarifa inatolewa kwamba, Mkutano Mkuu wa ishirini na nne wa mwaka wa Benki ya Biashara ya DCB, utafanyika siku ya Ijumaa tarehe 26 Juni 2026 kwa njia ya mtandao, kuanzia saa nne kamili Asubuhi.

### AGENDA

1. Kufungua Mkutano Mkuu wa Mwaka
2. Kuridhia agenda ya Mkutano Mkuu wa Ishirini na nne wa mwaka
3. Kuthibitisha kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa 23 wa mwaka uliofanyika tarehe 19 Julai 2025
4 Kupokea na kuridhia utekelezaji wa yatokanayo na Mkutano Mkuu wa 23 wa mwaka
5 Kupokea na kuridhia
   - 5.1 Taarifa ya wakurugenzi ya mwaka ulioishia tarehe 31 Disemba, 2025
   - 5.2 Taarifa ya hesabu zilizokaguliwa za mwaka ulioishia tarehe 31 Disemba, 2025
   - 5.3 Taarifa ya mkaguzi huru ya hesabu zilizokaguliwa za mwaka ulioishia tarehe 31 Disemba, 2025
6. Kupokea taarifa ya kuisha kwa muda wa Wajumbe wa Bodi ya wakurugenzi.
7 Uchaguzi wa wajumbe wa Bodi ya wakurugenzi
8. Kupokea na kuidhinisha uteuzi wa Mkaguzi Huru wa hesabu kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 31 Disemba 2026.
9 Kupokea na kuridhia pendekezo la malipo ya ada kwa Wajumbe wa Bodi.
10 Kupanga tarehe ya Mkutano Mkuu wa ishirini na 25 wa Mwaka
11 Mengineyo
12 Kufunga mkutano

### MAELEZO

1. Wanahisa wanaotarajia kuhudhuria Mkutano Mkuu wanatakiwa wawe na CDS namba ambazo zinapatikana kwenye risiti ya uwekezaji wa hisa (depository receipt) au taarifa ya akaunti (CSDR account statement).

2. Wanahisa ambao hawataweza kuhudhuria Mkutano wanaruhusiwa kuchagua wawakilishi watakaohudhuria na kupiga kura kwa niaba yao kwa kufuata/kuzingatia sheria na Katiba ya Kampuni. Fomu ya uwakilishi (Proxy Form) lazima ijazwe na kuwasilishwa kwenye ofisi ya Katibu wa benki iliyopo Makao Makuu ya benki ya DCB au kwa njia ya mtandao kupitia barua pepe shareholder@dcb.co.tz au matawini kabla ya saa 4 asubuhi siku ya Alhamisi tarehe 25 Juni 2026.

3. Nakala za taarifa ya mwaka na fomu za mwakilishi (proxy forms) zitapatikana matawini na kwenye tovuti ya benki (www.dcb.co.tz).

4. Orodha ya wanahisa itafungwa tarehe 22 Juni 2026.

5. Mapendekezo ya wanahisa yawasilishwe makao makuu ya benki ya DCB yaliyopo Magomeni Mwembechai au kwa barua pepe shareholder@dcb.co.tz kabla Jumatano tarehe 24 Juni 2026 saa 8.00 mchana.

Kwa idhini ya Bodi,

Regina Mduma

**Katibu wa Kampuni**

## 24.3 KUTHIBITISHA KUMBUKUMBU ZA MKUTANO MKUU WA 23 MWAKA ULIOFANYIKA TAREHE 19 JULAI 2025

Muhtasari wa Mkutano Mkuu wa 23 wa wanahisa wa benki ya biashara ya DCB uliofanyika tarehe 19 Julai 2025 kwa njia ya mtandao.

### WAJUMBE WA BODI WALIOHUDHURIA

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Bi. Zawadia Nanyaro | Mwenyekiti wa Mkutano |
| 2. | Bw. Alexander Sanga | Mjumbe wa Bodi |
| 3. | Prof. (Emer) Tadeo Satta | Mjumbe wa Bodi |
| 4. | Bw. David Shambwe | Mjumbe wa Bodi |
| 5. | Bi. Pamela Nchimbi | Mjumbe wa Bodi |
| 6. | Dkt. Amina Baamary | Mjumbe wa Bodi |
| 7. | Bw. Cliff Maregeli | Mjumbe wa Bodi |
| 8. | Bw. David Minja | Mjumbe wa Bodi |
| 9. | Bw. Onesmo Mwoga | Mjumbe Mbadala wa Bodi |
| 10. | Bw. Sabasaba Moshingi | Mkurugenzi Mtendaji |

### WAJUMBE WA BODI WALIOTOA UDHURU

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Bi. Hanifa Hamza | Mjumbe wa Bodi |

### SEKTRETARIETI

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Bi. Regina Mduma | Katibu wa benki |
| 2. | Bw. Alex Mgongolwa | Mwanasheria Mshauri wa benki |

### WAKURUGENZI WAANDAMIZI WA BENKI YA DCB

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Bw. Sabasaba Moshingi | Mkurugenzi Mtendaji |
| 2. | Bw. Leonard Katamba | Mkurugenzi wa Idara ya Uendeshaji na Tehama |
| 3. | Bi. Regina Mduma | Mkurugenzi wa Idara ya Sheria na Katibu wa benki |
| 4. | Bw. Deogratius Thadei | Mkurugenzi wa Idara ya Mikopo |
| 5. | Bi. Msingo Mkanzabi | Mkurugenzi wa Idara ya Rasilimali Watu |
| 6. | Bw. Ramadhan Mganga | Mkurugenzi wa Idara ya Biashara |
| 7. | Bi. Bertha Munyera | Mkurugenzi wa Idara ya Fedha |
| 8. | Bw. Emmanuel Barenga | Mkurugenzi wa Idara ya Ukaguzi wa Ndani |
| 9. | Bw. Emmanuel Mushi | Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Udhibiti wa Viashiria Hatarishi |

### WAWAKILISHI KUTOKA KUNDI LA WANAHISA WAANZILISHI

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Bw. Mpossi Gwakisa | Halmashauri ya Jiji la Dar-es-Salaam |
| 2. | Bw. Mpossi Gwakisa | Halmashauri ya Manispaa ya Ilala |
| 3. | Bw. Onesmo Mwoga | Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni |
| 4. | Bw. Daudi Mtatiro | Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo |
| 5. | Bw. Yahya Madenge | Halmashauri ya Manispaa ya Temeke |
| 6. | Bw. Rajab Gundumu | Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni |

### WAWAKILISHI KUTOKA KUNDI LA WANAHISA WA TAASISI

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Bw. Ronaldo Daniely | UTT-Asset Management & Investors' Services Plc |
| 2. | Bw. Mahmoud Seif | Public Service Social Security Fund (PSSSF) |
| 3. | Bw. Godson Kimbi | National Social Security Fund (NSSF) |
| 4. | Bw. David Sikaponda | National Health Insurance Fund |

### WANAHISABINAFSI

**Orodha imeambatanishwa kama Kiambatanisho 1**

### WAALIKWA

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Bw. Frank Mboya | Mkaguzi Huru – KPMG |
| 2. | Bi. Mariam Mtunguja | Mamlaka ya Masoko ya Mtaji na Dhamana |
| 3. | Bi. Ester Mwamwala | Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) |
| 4. | Bi. Eunice P. Mwasa | Benki Kuu |



Benki Kidijitali. Bila Makato. Bila Mipaka.

### AGENDA 1: KUFUNGUA MKUTANO MKUU WA MWAKA

Katibu wa benki, kwa kushirikiana na Mwanasheria Mshauri wa benki, walithibitisha kuwa kwa mujibu na Sheria ya Makampuni ya Tanzania pamoja na Katiba ya benki, Mkutano Mkuu ulihitaji akidi ya asilimia 75 ya wanahisa. Akidi ya zaidi ya asilimia 80 ilithibitishwa na hivyo Mkutano Mkuu ulifunguliwa rasmi saa nne na robo asubuhi.

### AGENDA 2: KURIDHIA AGENDA YA MKUTANO MKUU WA 23 WA MWAKA

Katibu wa benki kwa kushirikiana na Mwanasheria Mshauri wa benki walithibitisha kuwa taarifa ya Mkutano Mkuu wa 23 wa Mwaka ilitolewa kwa wanahisa wote zaidi ya siku ishirini na moja kabla ya Mkutano huo kupitia magazeti, mitandao ya kijamii, tovuti ya benki na ujumbe mfupi wa maandishi (SMS). Kwa kuwa Katibu wa Kampuni hajapokea mapendekezo yeyote ya mabadiliko ya agenda, hivyo basi agenda ya Mkutano Mkuu wa 23 wa Mwaka iliyotangazwa ndio agenda iliyotumika katika kikao hicho.

Wanahisa waliridhia agenda ya Mkutano Mkuu wa 23 wa Mwaka kama ilivyochapishwa bila mabadiliko yeyote.

### AGENDA 3: KUTHIBITISHA KUMBUKUMBU ZA MKUTANO MKUU WA 22 WA MWAKA

Wajumbe wa Mkutano Mkuu walipitishwa kwenye kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa 22 wa Mwaka na waliridhia kumbukumbu hizo bila mapendekezo au maboresho yeyote.

### AGENDA 4: KUPOKEA, KUJADILI NA KURIDHIA TAARIFA UTEKELEZAJI WA YATOKANAYO NA MKUTANO MKUU WA 22 WA MWAKA

Wanahisa waliridhia rasmi utekelezaji wa maazimio na maagizo yote yaliyotolewa katika Mkutano Mkuu wa 22 wa Mwaka.

### AGENDA 5: TAARIFA YA WAKURUGENZI NA TAARIFA YA HESABU ZILIZOKAGULIWA KWA MWAKA ULIOISHIA TAREHE 31 DISEMBA, 2024

5.1 Wanahisa walipokea taarifa kutoka kwa Bodi ya Wakurugenzi iliyojumuisha barua ya Mwenyekiti wa Bodi, barua ya Mkurugenzi Mtendaji, taarifa za fedha za mwaka ulioishia tarehe 31 Disemba 2024, pamoja na taarifa ya Mkaguzi Huru wa Mahesabu.

5.2 Ilielezwa kuwa jumla ya Wakurugenzi kumi (10), akiwemo Mkurugenzi Mtendaji, walihudumia katika Bodi ya benki kwa mwaka 2024 na hakuna mjumbe wa bodi aliyemiliki hisa zenye thamani ya zaidi ya asilimia 5 ya mtaji wa benki. Wakurugenzi hao walitekeleza majukumu yao kama ilivyoainishwa kwenye Katiba ya benki, sheria na kanuni mbalimbali za wathibiti wa benki.

5.3 Iliripotiwa kuwa katika mwaka 2024, benki ilipiga hatua muhimu katika utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Miaka Mitano (2024–2028), ambapo matokeo chanya yalianza kuonekana. Mahesabu yaliyokaguliwa yalionyesha kwamba hasara ya benki ilipungua kutoka Tsh bilioni 4.59 kabla ya kodi mwaka 2023 hadi kufikia Tsh bilioni 1.7 kabla ya kodi kwa mwaka 2024.

5.4 Iliripotiwa kuwa mapato yatokanayo na riba yaliongezeka kwa asilimia 16 hadi kufikia Tsh bilioni 32.28, yakichangiwa na mikopo ya Tsh bilioni 24.87. Hata hivyo, gharama za riba ziliongezeka kwa asilimia 27 kutoka Tsh bilioni 15.09 mwaka 2023 hadi Tsh bilioni 19.23 mwaka 2024, hali hii ilitokana na changamoto za ukwasi pamoja na gharama za kuongeza mtaji.

5.5 Iliripotiwa kuwa mizania ya benki iliendelea kuwa imara ambapo jumla ya mali ziliongezeka kwa asilimia 12.2 kutoka kiasi cha Tsh bilioni 230.9 hadi kufikia Tsh bilioni 259.1. Ukuaji huu ulichangiwa na ongezeko la mikopo pamoja na uwekezaji katika hatifungani za serikali. Aidha, amana za wateja ziliongezeka kwa asilimia 8.6 kutoka kiasi cha Tsh bilioni 140 hadi kufikia Tsh bilioni 152.

5.6 Iliripotiwa kuwa mtaji wa benki uliimarika kufuatia mafanikio ya zoezi la uuzaji wa Hisa Stahiki, ambapo uwiano wa mtaji wa daraja la kwanza ulifikia asilimia 15.68 na daraja la pili asilimia 16.03. Vilevile, ufanisi wa kiutendaji uliimarika ambapo uwiano wa gharama kwa mapato ulipungua kutoka asilimia 108 mwaka 2023 hadi asilimia 97.98 mwaka 2024. Faida kwa kila hisa (ROE) nayo iliongezeka kutoka asilimia -22 hadi asilimia -0.93.

5.7 Iliripotiwa kuwa, benki ilifanikiwa kukusanya zaidi ya Tsh bilioni 10 kupitia uuzaji wa Hisa Stahiki, zoezi lililovutia wawekezaji wapya wa kimkakati. Hatua hii ilisaidia kuimarisha ukwasi wa benki na kuongeza uwezo wake wa kupata amana kwa gharama nafuu.

5.8 Iliripotiwa kuwa mikopo kwa wateja iliongezeka kwa asilimia 9.97, hasa katika sekta ya biashara ndogo ndogo na za kati (MSMEs na SMEs). Aidha, benki iliendelea kuimarisha mifumo ya kutoa huduma kwa njia za kidijitali ili iweze kuwafikia wateja wengi zaidi nchini.

5.9 Wanahisa walijulishwa kwamba mwaka 2025 unatarajiwa kuwa na mafanikio makubwa kutokana na kuimarika kwa mtaji wa benki, kuboreshwa kwa utawala, na uwepo wa mpango mkakati thabiti. Benki imepanga kuongeza utoaji wa mikopo, kupanua vyanzo vya mapato yasiyotokana na riba kupitia huduma za kidijitali, kuboresha ufanisi wa kiutendaji kwa kutumia teknolojia na kukuza ujumuishi wa kifedha kwa makundi mbalimbali huku ikizingatia misingi ya ESG.

5.10 Mkaguzi Huru wa Mahesabu kutoka KPMG alithibitisha kuwa taarifa za fedha ziliandaliwa kwa kuzingatia viwango vya kimataifa vya uhasibu, kanuni za Benki Kuu ya Tanzania, na sheria husika. Aidha, Mkaguzi Huru alitoa hati safi ya ukaguzi na kuthibitisha kuwa hali ya kifedha ya benki iko imara.

***Baada ya uwasilishaji wa taarifa ya Bodi ya Wakurugenzi na taarifa ya Mkaguzi Huru wa mahesabu, wanahisa walipokea taarifa hiyo, kuijadili kwa kuuliza maswali, kutoa maoni, maelekezo na mapendekezo kama inavyoonekana hapa chini.***

i. **ILIPENDEKEZWA** kwamba benki iweke kipaumbele katika kuimarisha huduma za kidijitali. Mwanahisa alisisitiza kwamba huduma hizo zitaweza kuwasaidia wateja wa benki hasa wale wanaosafiri nje ya nchi na kufanya malipo kwa njia ya mtandao.

**MAELEZO:** Benki inaelekeza nguvu kubwa katika kuboresha huduma za kidijitali ili kuwafikia wateja wengi zaidi kwa urahisi. Katika mpango wa benki wa miaka mitano, moja ya vipaumbele vikuu ni kuimarisha mifumo ya kidijitali. Kupitia huduma hizi, mteja anaweza kufanya malipo akiwa popote duniani, hasa kwa kuwa benki ni mshirika wa huduma za VISA, hivyo huduma za malipo zinapatikana kimataifa bila matatizo. Aidha, benki inatoa huduma kwa njia ya mtandao na simu ya mkononi (internet banking na mobile banking) zinazomwezesha mteja kuhamisha fedha na kufanya malipo akiwa mahali popote.

ii. **SWALI:** Taarifa zinaonesha kuwa kiwango cha mikopo chechefu (NPL) ni asilimia 4.96, ambacho ni karibu sana na ukomo wa asilimia 5 uliowekwa na Benki Kuu ya Tanzania. Benki imeweka mikakati gani Ili kuhakikisha kiwango hiki kinaendelea kushuka zaidi.

**JIBU:** Kati ya mwaka 2023 hadi 2025, benki imefanikiwa kupunguza mikopo chechefu kwa kiasi kikubwa kupitia utekelezaji wa mikakati mbalimbali ikiwemo; kuimarisha uchambuzi wa mikopo, kuongeza ufuatiliaji wa mikopo baada ya kutoa mikopo hiyo na kuchukua hatua stahiki kwa wakati. Aidha, matumizi ya teknolojia yameboreshwa ili kuongeza ufanisi katika tathmini na usimamizi wa hatari zitokanazo na mikopo.

iii. **ILIAGIZWA** kwamba mpango mkakati wa benki wa miaka mitano uwe na mkakati maamulu wa kuongeza mapato, kupunguza matumizi, na kuweka uwiano mzuri kati ya mapato na gharama ili kuweza kufikia uwiano uliowekwa na Benki Kuu, yaani asilimia 55.

iv. **ILIPENDEKEZWA** kwamba benki iangalie upya sera zake ili kuona namna bora ya kuwapatia mikopo wanahisa waanzilishi yaani halmashauri za manispaa za Dar es Salaam, kupitia miradi mbalimbali kwa manufaa ya pande zote mbili. Ushirikiano huo unaweza kusaidia kuimarisha mapato ya benki kupitia mikopo na uwekezaji katika miradi ya Halmashauri.

v. **SWALI:** Wanahisa wapya wategemee nini kwa mwaka 2025 na Mkutano Mkuu wa 24.

**JIBU:** Benki bado ipo katika kipindi cha mabadiliko na kujijenga upya. Ilielezwa kuwa uwekezaji katika hisa ni wa muda mrefu, na uongozi unaendelea kuomba muda zaidi ili kuimarisha taasisi pamoja na kuboresha ufanisi wake wa kifedha. Aidha, mabadiliko yanayoendelea yanalenga kuhakikisha kuwa wanahisa watanufaika kupitia magawio, sambamba na ongezeko la thamani ya hisa litakalotokana na ukuaji wa benki na kuimarika kwa utendaji wake kibiashara.

vi. **ILIPENDEKEZWA** kwamba katika Mkutano Mkuu wa wanahisa kuwe na agenda ya gawio ambayo ni mojawapo ya sababu kuu inayosukuma watu kuwekeza katika benki.

**JIBU:** Benki ilipokea pendekezo hilo na kueleza kuwa agenda ya gawio inapatikana ndani ya taarifa ya wakuregenzi wa Bodi. Imekuwa desturi ya DCB kueleza mapendekezo ya Bodi kuhusu gawio kupitia barua ya Mwenyekiti wa Bodi. Wanahisa upewa muda wa kutosha wa kujadili taarifa ya wakurugenzi wa Bodi kuhusu mwendendo wa gawio na uendelevu.

vii. **ILISHAURIWA** kwamba benki ifikirie juu ya kutoa mikopo kwa njia ya mtandao kwenye akaunti zinazofanya miamala mingi ili kuwapa hamasa wateja wake.

**JIBU:** Benki ilimshukuru mwanahisa kwa pendekezo hilo na kueleza kwamba mteja anayepitisha mshahara wake DCB anaweza kukopa kidijitali hadi asilimia hamsini ya mshahara huo.





## AGENDA 6: KUPOKEA NA KURIDHIA MABADILIKO YA VIFUNGU VYA KATIBA YA KAMPUNI

6.1 Mkutano ulijadili mapendekezo ya marekebisho ya Katiba ya Kampuni yanayolenga kuboresha uwakilishi wa wanahisa katika Bodi ya Wakurugenzi kulingana na umiliki wa hisa katika benki. Ilipendekezwa kuwa kila kundi la wanahisa liwe na haki ya kuchagua wawakilishi wake ili kuhakikisha ushiriki wa moja kwa moja katika maamuzi ya kimkakati na kuakisi maslahi yao ndani ya Bodi. Pia mjumbe huru wa bodi (independent cluster) atachaguliwa na wanahisa wote.

6.2 Kwa upande wa wanahisa wa taasisi, ilipendekezwa kuwa kundi hilo liwe na haki ya kuwa na hadi Wakurugenzi wanne endapo umiliki wao hautashuka chini ya asilimia 35 ya mtaji wa benki, huku kila taasisi inayotaka uwakilishi ikitakiwa kumiliki angalau asilimia 5 ya hisa za benki. Hata hivyo, kila taasisi itakuwa na haki ya nafasi moja tu ya uwakilishi katika Bodi. Marekebisho haya yamelenga kutoa nafasi kwa wawekezaji wapya waliopatikana kupitia zoezi la Hisa Stahiki la mwaka 2024, kuwa na wawakilishi katika Bodi ya Wakurugenzi ya benki.

6.3 Ilipendekezwa kuwa idadi ya Wakurugenzi kutoka kundi lolote la wanahisa iwe inarekebishwa kulingana na mabadiliko ya umiliki wa hisa, na mabadiliko hayo yatahitaji idhini ya wanahisa kupitia Mkutano Mkuu. Kwa ujumla, marekebisho ya Katiba yalilenga kanuni za utawala bora, uwazi, na uwakilishi wa haki ndani ya Bodi ya Wakurugenzi.

***Wanahisa walipokea na kuidhinisha mabadiliko ya vifungu vya katiba ya kampuni.***

## AGENDA 7: KURIDHIA UTEUZI WA WAJUMBE WA BODI

7.1 Iliripotiwa kuwa katika zoezi la Hisa Stahiki la mwaka 2024, taasisi mbili za mifuko ya hifadhi ya jamii, Public Service Social Security Fund (PSSSF) na National Social Security Fund (NSSF), zilijiunga na benki kama wanahisa wakubwa, zikiwa na umiliki wa asilimia 9.71 na 5.21 mtawalia. Kwa mujibu wa Katiba ya benki Ibara ya 56 (4), taasisi zenye umiliki wa angalau asilimia 5 zinastahili uwakilishi katika Bodi ya Wakurugenzi, huku kila taasisi ikiwa na haki ya nafasi moja ya uwakilishi.

7.2 Bodi ilipendekeza Mkutano Mkuu uidhinishe uteuzi wa wajumbe wawili wa Bodi, mmoja kutoka PSSSF na mmoja kutoka NSSF, kwa sharti la kupata idhini ya Benki Kuu ya Tanzania kabla hawajaanza kuhudumia katika benki.

***Wanahisa waliidhinisha uteuzi wa wajumbe wa Bodi kutoka PSSSf na NSSF kwa sharti la kupata idhini ya Benki Kuu ya Tanzania kabla ya kuanza kuhudumia benki.***

## AGENDA 8: KUTEUA MKAGUZI HURU WA MAHESABU KWA MWAKA UNAOISHIA 31 DISEMBA 2025

8.1 Iliripotiwa kuwa Wakaguzi kutoka KPMG Tanzania walionyesha utayari wa kuendelea kutoa huduma za ukaguzi kwa mwaka wa fedha unaoishia 31 Disemba 2025 kwa gharama ileile ya Tsh 140,989,527.00, ikiwa ni mwaka wao wa pili wa kuhudumia benki. Ilielezwa kuwa kwa mujibu wa sheria na kanuni husika, kampuni hiyo bado inaweza kuendelea kuwa Mkaguzi Huru wa Hesabu.

8.2 Iliripotiwa kuwa kwa kuzingatia kuwa mamlaka ya kuteua Mkaguzi Huru wa Hesabu yapo kwa Mkutano Mkuu wa Wanahisa, Bodi ya Wakurugenzi ilipendekeza wanahisa waidhinishe uteuzi wa KPMG Tanzania kama Mkaguzi Huru wa mahesabu na mifumo ya TEHAMA ya benki kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 31 Disemba 2025.

***Wajumbe waliidhinisha pendekezo la Bodi na kumteua KPMG Tanzania kama Mkaguzi Huru wa Fedha kwa mwaka wa fedha unaoishia 31 Disemba 2025 kwa kiasi cha Tsh 140,989,527.***

## AGENDA 9: KUPOKEA NA KURIDHIA PENDEKEZO LA MALIPO YA ADA KWA WAJUMBE WA BODI

Wanahisa waliidhinisha pendekezo la Bodi la malipo ya ada kwa Wajumbe wa Bodi kuendelea kuwa Tsh 6,000,000 baada ya kodi kwa mwaka kwa kila Mjumbe wa Bodi.

## AGENDA 10: KUPANGA TAREHE YA MKUTANO MKUU WA ISHIRINI NA NNE

Wanahisa waliazimia kuwa Mkutano Mkuu wa Ishirini na nne wa mwaka ufanyike siku ya Ijumaa tarehe 26 Juni 2026.

**AGENDA 11: MENGINEYO**

**ILIRIPOTIWA** kwamba hakukuwa na agenda ya mengineyo iliyowakilishwa kwa Katibu wa Kampuni kabla ya Mkutano Mkuu na pia wanahisa hawakuwa na mengineyo yeyote.

Mkutano ulifungwa saa 7:00 mchana.



26 Juni 2026

**Zawadia Nanyaro** **Tarehe**

**Mwenyekiti**



26 Juni 2026

**Regina Mduma** **Tarehe**

**Katibu wa Kampuni**





## 24.4 KUPOKEA NA KURIDHIA UTEKELEZAJI WA YATOKANAYO NA MKUTANO MKUU WA 23 WA MWAKA

Yatokanayo na Mkutano Mkuu wa 23 wa Mwaka uliofanyika tarehe 19 Julai 2026

| AGIZO | UTEKELEZAJI |
|---|---|
| Mpango mkakati wa benki wa miaka mitano ulenge kwenye kuongeza mapato, kupunguza matumizi, na kuweka uwiano mzuri kati ya mapato na gharama ili kuweza kufikia uwiano wa asilimia 55 uliowekwa na Benki Kuu. | Bodi inaendelea kuisimamia menejimenti katika utekelezaji wa mpango mkakati wa miak mitano (2024-2028) na agizo la wanahisa lipo ndani ya Mpango makati huo. Yafuatayo yalitekelezwa ndani ya mwaka 2025:<br>(i) Mtaji wa benki umeendelea kuwa imara na kukidhi matakwa ya Benki Kuu,<br>(ii) Gharama zimepungua kwa asilimia 4,<br>(iii) Huduma zinazotolewa kijiditali zimeongezeka. Mteja anaweza kujifungulia akaunti mwenyewe kupitia App ya DCB Pesa Plus bila kufika tawini.<br>(iv) Amana za benki za gharama nafuu ziliongezeka kutoka asilimia 27.5 hadi kufikia asilimia 34.2 |

Benki Kidijitali. Bila Makato. Bila Mipaka.

## 24.5 KUPOKEA NA KURIDHIA TAARIFA:

### 24.5.1 Barua ya mwenyekiti wa Bodi kwa wanahisa



**MALI ZA BENKI**

**Tsh 260.8B ▲**

**THAMANI YA HISA**

**Tsh 47B ▲**

**Ndugu wanahisa,**

Ninayo furaha kuwasilisha Ripoti ya benki na Taarifa ya Fedha ya mwaka 2025. Mwaka huu umekuwa mzuri sana kwa benki yetu ya DCB, kwa matokeo yake thabiti kifedha na kiutendaji yanayoakisi mikakati bora na utekelezaji wenye ufanisi na kuongeza thamani ya muda mrefu ya wanahisa.

#### Hali ya Uchumi kwa Mwaka 2025

Mazingira ya uendeshaji biashara nchini Tanzania katika mwaka 2025 yaliendelea kuwa imara ikiashiria msingi thabiti wa uchumi katika sekta ya fedha. Uchumi ulikuwa kwa wastani wa asilimia 5.9 na 6.4, ukichochewa na utendaji mzuri wa sekta za kilimo, madini, ujenzi, utalii na huduma za kifedha, sambamba na uwekezaji katika miradi ya kimkakati ya miundombinu na shughuli za sekta binafsi. Mfumuko wa bei uliendelea kuwa tulivu kati ya asilimia 3.2 na 3.6, jambo linalodhihirisha ufanisi wa sera za fedha na usimamizi madhubuti wa uchumi. Aidha, ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi uliendelea kuimarika na kufikia kati ya asilimia 20 na 23.5, ukiongozwa na sekta za madini, biashara na kilimo. Riba za mikopo zilishuka hadi wastani wa asilimia 15.2 na hivyo kuboresha upatikanaji wa huduma za kifedha. Kwa ujumla, mwenendo huu unaakisi uthabiti wa uchumi ambao ulileta mazingira wezeshi kwa benki ya DCB kutekeleza mikakati yake kwa mwaka 2025.

#### Utendaji wa DCB kwa Mwaka wa Fedha 2025

Kwa mwaka wa fedha 2025, benki iliendelea kuwa na utendaji bora na ufanisi ambapo hasara ya benki kabla ya kodi ilipungua kutoka Tsh bilioni 1.7 kwa mwaka 2024 hadi kufikia Tsh milioni 347, ambayo ni sawa na punguzo la hasara kwa asilimia 80. Mafanikio haya yanadhihirisha kuimarika kwa shughuli za msingi za benki, udhibiti makini wa gharama pamoja na uthabiti katika mazingira yenye ushindani. Licha ya kuwepo kwa changamoto mbalimbali zilizotokana na misukosuko ya kiuchumi duniani na kuyumba kwa masoko ya kimataifa ya kifedha, benki iliendeshwa katika mazingira tulivu ya kibiashara.

Aidha, wastani wa faida ya mtaji iliongezeka kwa asilimia moja kutoka -3.5 mwaka 2024 hadi asilimia -2.5 mwaka 2025. Hii inaashiria matumizi bora ya mtaji na mwelekeo chanya katika kuongeza thamani kwa wanahisa.

Jumla ya mali za benki zilifikia Tsh bilioni 260.8, ambapo mikopo iliyotolewa na amana za wateja zilifikia Tsh bilioni 133.7 na Tsh bilioni 150, mtawalia. Aidha, benki iliendelea kudumisha viwango imara vya ukwasi kwa asilimia 25 na mtaji kwa asilimia 16.32. Hali hii inaakisi ustahilimivu wa kifedha na uzingatiaji wa matakwa ya kisheria.

#### Soko na Thamani kwa Wanahisa

Imani ya wawekezaji iliendelea kuwa imara, huku thamani ya hisa ya DCB sokoni (Market Capitalization) iliongezeka kutoka Tsh bilioni 39 mwaka 2024 hadi kufikia Tsh bilioni 47 mwaka 2025, na bei ya hisa ilipanda kutoka Tsh 135 kwa hisa mpaka Tsh 240. Hii inaashiria kuongezeka kwa imani ya wanahisa wetu katika mikakati ya benki. Hata hivyo, kufikia tarehe 31 Mei 2026, bei ya hisa moja ya benki sokoni ilikuwa Tsh 535 na thamani ya hisa ya DCB sokoni ilikuwa Tsh bilioni 102.

#### Pendekezo la Gawio

Kwa kuzingatia matokeo ya mwaka wa fedha 2025 na matakwa ya kanuni za uthibiti, Bodi inawafahamisha wanahisa kwamba benki haitaweza kutoa gawio kwa mwaka huu. Hata hivyo, Bodi inaendelea kusimamia mpango mkakati wake unaolenga ukuaji wa benki, kuimarisha utendaji na kujenga misingi imara ya kuongeza thamani kwa wanahisa katika kipindi kijacho.

#### Nafasi ya Bodi katika Usimamizi wa Kimkakati

Mwaka 2025 ulikuwa muhimu katika kuimarisha msingi wa ukuaji wa benki kwa miaka ijayo. Katika kipindi hicho, Bodi iliendelea kutoa mwongozo wa kimkakati kwa Menejimenti kwa lengo la kuhakikisha uendelevu wa biashara, kuimarisha mifumo ya utawala bora, kuboresha usimamizi wa viashiria hatarishi na kusimamia uwekezaji katika teknolojia, kuharakisha mageuzi ya kidijitali yanayoongeza ufanisi na kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa wateja.

Bodi ina matarajio makubwa kuhusu utekelezaji wa mkakati wa mwaka 2026 unaolenga kuongeza mapato, kupunguza gharama za fedha, kuboresha ufanisi wa matumizi ya rasilimali na kupunguza kiwango cha mikopo chechefu. Tunaamini kuwa utekelezaji wa mkakati huu utairejesha benki katika kupata faida endelevu, kuimarisha mtaji wake na kuongeza thamani kwa wanahisa.

#### Utawala Bora na Uzingatiaji wa Sheria na Kanuni

Utawala bora umeendelea kuwa nguzo muhimu katika kuhakikisha uthabiti, uwajibikaji na uendelevu wa benki. Katika mwaka wa fedha 2025, Bodi iliendelea kusimamia mifumo ya viashiria hatarishi, ukaguzi na udhibiiti wa ndani ili kuhakikisha shughuli za benki zinaendeshwa kwa uwazi na uwajibikaji. Pia Bodi ilihakikisha uwepo wa mifumo mathubuti yakusimamia uadilifu wa taarifa za benki, tathmini ya utendaji wa viongozi na mpango wa kurithisha majukumu ya uongozi unabaki imara na wenye kuendana na mahitaji ya sasa na ya baadaye. Haya yote yalitekelezwa kupitia Kamati za Bodi za mikopo, Ukaguzi, Utawala Bora na Rasilimali Watu.

Sambamba na hilo, benki iliendelea kuimarisha mazingira ya udhibiti kupitia tathmini za robo mwaka, uzingatiaji wa sheria na kanuni pamoja na usimamizi wa ukaguzi huru wa nje. Hatua hizi zimeendelea kuimarisha imani ya wanahisa, wateja, wadhibiti na wadau wengine katika uadilifu wa taarifa za fedha na uimara wa mifumo ya utawala wa benki.

#### Mazingira, Jamii na Utawala Bora (ESG)

Katika mwaka uliopita, benki iliendelea kuzingatia misingi ya Mazingira, Jamii na Utawala Bora (ESG) katika utekelezaji wa shughuli zake, kwa kuimarisha ujumuishi wa kifedha, utoaji wa mikopo kwa uwajibikaji na ushiriki katika maendeleo ya jamii. Miongoni mwa hatua zilizotekelezwa ni pamoja na kuongeza huduma za mawakala wa benki katika maeneo ambayo hayakuwa na huduma za kutosha za kifedha, kusaidia biashara ndogo na za kati pamoja na wajasiriamali wadogo kupitia suluhisho mahsusi, na kujumuisha masuala endelevu katika michakato ya utoaji wa mikopo na manunuzi. Aidha, benki iliendelea kuimarisha utawala bora na kuendeleza maadili ya uwajibikaji katika utekelezaji wa shughuli zake.

Sambamba na dhamira yetu ya kukuza ujumuishi wa kifedha, benki iliendelea kuwahudumia na kuwawezesha wanawake kupitia bidhaa yake maalum ya mikopo inayolenga wanawake wajasiriamali wadogo, pamoja na kuendelea kutoa huduma za kifedha zinazokidhi mahitaji ya vijana. Juhudi hizi zimeendelea kupanua upatikanaji wa mikopo nafuu na kuchochea ushiriki wa makundi mbalimbali ya jamii katika shughuli za kiuchumi, hivyo kuchangia maendeleo jumuishi na endelevu ya Taifa letu.

#### Mtazamo wa Baadaye

Katika kipindi kijacho, DCB itaendelea kulinda mapato yake, kuimarisha mtaji na kudumisha mifumo ya usimamizi ya viashiria hatarishi ili kuhakikisha uthabiti na ukuaji endelevu katika mazingira yenye ushindani mkubwa. Uchumi wa Tanzania unatarajiwa kuendelea kukua huku pato la Taifa likikadiriwa kufikia kati ya asilimia 5.3 hadi 5.5 mwaka 2026, ukichangiwa na utendaji imara katika sekta za kilimo, ujenzi, utalii, madini na huduma. Mtazamo huu mzuri wa kiuchumi unatoa mazingira ya kuunga mkono upanuzi wa sekta ya benki, na DCB iko katika nafasi nzuri ya kutumia fursa hizi.

#### Shukurani

Kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi, natoa shukurani zangu za dhati kwa wanahisa wetu kwa kuendelea kutuamini na kutuunga mkono, kwa wateja wetu kwa uaminifu na ushirikiano wao, kwa mamlaka za usimamizi kwa mwongozo na msaada wao, na kwa wafanyakazi wote wa benki kwa kujituma na kujitoa kwao katika safari ya kuirejesha benki katika mafanikio.

Uaminifu mliouonyesha kwa benki mwaka 2025, licha ya changamoto tulizopitia ni ushahidi tosha wa imani na ushirikiano wetu sote kama wadau wa DCB. Kwa pamoja, tutaendelea kujenga benki yenye misingi imara, inayoongeza thamani kwa wanahisa wetu na kutoa mchango wa kudumu katika safari ya maendeleo ya uchumi wa Tanzania.

Wenu katika Utumishi,

Bi. Zawadia J. Nanyaro

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi

## 24.5.2 Taarifa ya Mkurugenzi Mtendaji



**HATUA KUBWA KATIKA KUPUNGUZA HASARA NA KUBORESHA UFANISI**




| 2024 | 2025 |
|---|---|
| TZS 1.7 BILIONI | TZS 347 MILIONI |
| HASARA | HASARA |

Mafanikio makubwa ikilinganishwa na hasara kabla ya kodi.

**Ndugu Wanahisa,**

Kwa niaba ya Menejimenti ya benki ya biashara ya DCB, ninafuraha kuwasilisha ripoti ya mwaka 2025 inayotoa muhtasari wa utendaji wetu na utekelezaji wa mpango mkakati na matarajio ya siku zijazo.

**Muhtasari wa Utendaji wa Benki**

Mwaka wa fedha ulioishia 31 Disemba 2025, benki ilifanya vizuri na kupunguza hasara kabla ya kodi kutoka kiasi cha Tsh bilioni 1.7 mwaka 2024 hadi kufikia Shilingi za Kitanzania milioni 347. Hii ni sawa na punguzo la hasara kwa asilimia 80. Hii inaonyesha juhudi za mkakati wetu na dhamira yetu ya kuendeleza ukuaji endelevu.

Amana za benki za gharama nafuu ziliongezeka kutoka asilimia 27 mwaka 2024 hadi kufikia asilimia 34.2. Matokeo haya chanya yanaonyesha kazi kubwa iliyofanywa na benki katika kutekeleza mpango mkakati wake wa kuongeza amana za gharama nafuu zinazolenga kupunguza gharama za uendeshaji. Gharama za uendeshaji zilipungua kutoka asilimia 104.7 mwaka 2024 hadi kufikia asilimia 94.08. Hii inaonyesha ustahimilivu wa hali ya juu katika shughuli za benki.

Katika kipindi chote cha mwaka, tuliboresha uwezo wa kidijitali, kuongeza wigo wa upatikanaji wa huduma za kifedha, kuwezesha wafanyabiashara wadogo na wa kati na kuanzisha huduma kulingana na mahitaji ya wateja wetu; juhudi ambazo zililenga kurahisisha upatikanaji wetu na kuhamasisha ujumuishaji wa kifedha nchini.

**Maendeleo katika Utekelezaji wa Vipaumbele vya Kimkakati**

Kipaumbele muhimu cha kimkakati katika mwaka 2025 kilikuwa kuendeleza agenda yetu ya mageuzi ya kidijitali chini ya kaulimbiu ya Benki Kidijitali, Bila Makato, Bila Mipaka.

Kwa mwaka uliopita, tuliongeza uwekezaji katika teknolojia na njia za utoaji huduma za kidijitali ili kuwapatia wateja huduma za kifedha zilizo bora, salama, na nafuu. Tuliimarisha Internet Banking, DCB Pesa Plus, huduma za mawakala, ilikuongeza urahisi wa kufanya miamala na upatikanaji wa huduma. Mipango hii ni muhimu katika kujenga msingi imara utakaowezesha benki kujiweka katika nafasi bora ya ushindani na kunufaika na fursa zinazojitokeza katika uchumi wa kidijitali unaokua kwa kasi nchini.

Benki ilipiga hatua muhimu katika utekelezaji wa mpango wake, ikiwa ni pamoja na kuimairisha mifumo ya usimaizi wa vihashiria hatarishi, ufuatiliaji na uhakiki wa ubora wa mikopo na ukusanyaji wa madeni. Aidha, benki iliendelea kuweka kipaumbele kwenye mafunzo na maendeleo ya wafanyakazi ili kuwajengea uwezo, ambao ni msingi muhimu katika kuboresha utoaji wa huduma.

Mipango mingine muhimu ya kimkakati kama vile kufungua akaunti kwa kutumia simu bila kufika tawini, ushirikiano na SACCOS na kampuni za teknolojia ya kifedha (Fintechs), iliendelezwa kwa lengo la kuongeza amana za gharama nafuu, vyanzo vya fedha, na





### VIPAUMBELE VYETU VIKUU VYA KIMKAKATI

| KUPATA WATEJA KWA KASI ZAIDI | KUKUZA AMANA ZA WATEJA CASA | KUKUZA KITABU CHA MIKOPO | KUIMARISHA UWEZO WETU WA KIDIGITALI | UWEKEZAJI KATIKA TEKNOLOJIA, UBUNIFU NA HUDUMA BORA. |
|---|---|---|---|---|
| Kuongeza idadi ya wateja kupitia mikakati mahsusi ya kuwafikishia, huduma zinazolenga mahitaji yao. | Kuimarisha uhusiano na wateja na kutoa huduma zenye thamani ili kuongeza amana za CASA. | Kuimairisha uchambuzi wa mikopo na kuongeza ufuatiliaji wa mikopo baada ya kutoa. | Kuwekeza katika teknolojia na kuongeza huduma zinazotolewa kidijitali. | Kuimarisha teknolojia, kukuza ubunifu na kutoa huduma bora ili kukidhi mahitaji ya wateja. |

Tumejidhatiti kujenga benki ya kisasa iliyo tayari kwa siku zijazo, yenye ustahimilivu na wepesi wa kukabiliana na mabadiliko, huku ikitoa thamani endelevu kwa wateja, wadau na

kupunguza utegemezi wa amana zenye gharama kubwa. Mipango hii ilichangia kupungua kwa uwiano wa gharama dhidi ya mapato na inaendelea kuimarisha uthabiti wa benki katika mazingira haya yenye ushindani mkubwa.

**Matarajio ya Mwaka 2026 na Kuendelea**

Mtazamo wetu wa kipindi kijacho ni kuendelea kuimarisha huduma zetu za kibenki, tukisimamia mapato, kulinda mtaji na usimamizi madhubuti wa viashiria hatarishi. Tutaendelea na mpango mkakati wetu wa kuongeza wateja wapya, kukuza amana na kitabu cha mikopo, kuongeza bidhaa zinazotolewa kidigitali ili tuweze kuhudumia wateja wetu kwa ufanisi zaidi. Tutaendelea kuwekeza kwenye tekinolojia, ubunifu na utoaji wa huduma bora ili kuhakikisha kubenki na DCB ni rahisi, salama, bila vikwazo na bila makato ili kukidhi matakwa ya wateja.

Mkakati wetu wa biashara utaendelea kuzingatia kanuni za mazingira, jamii na utawala bora hususani katika ujumuishi wa kifedha, kuimarisha misingi madhubuti ya utoaji huduma za kibenki na ushirikiano endelevu unaochangia maendeleo ya jamii.

Tunatambua kuwa wafanyakazi wetu ndio msingi muhimu wa mafanikio ya benki. Hivyo tutaendelea kuimarisha uwezo wa uongozi, kukuza vipaji vya wafanyakazi na kuwekeza katika maendeleo yao ili kujenga utamaduni wa uajibikaji, ubunifu na utendaji bora unaowezesha utekelezaji wa malengo yetu na kuendelea kuongeza thamani kwa wanahisa na wadau wetu.

**Shukurani**

Ninapenda kuwashukuru kwa dhati wanahisa wetu, kwa imani waliyoweka katika benki yetu, wateja wetu kwa kufanya biashara na sisi, mamlaka mbalimbali zinazotusimamia kwa miongozo yao, Bodi ya Wakurugenzi kwa kusimamia mpango mkakati wa benki yetu na wafanyakazi wenzangu kwa kujitolea kufanya kazi kwa bidii. Tunapoendelea na safari hii ya mageuzi nina imani kuwa tukishirikina pamoja tutafanya mabadiliko makubwa katika sekta ya benki na uchumi wa Tanzania.

Sabasaba Moshingi
Managing Director
**DCB Commercial Bank Plc**

## 24.5.3 Taarifa ya Mkurugenzi wa Fedha



**MIKOPO**

**Tsh 133.3B**
**kulinganisha na Tsh 132.4B (2024)**

**ONGEZEKO LA CASA**

Uwiano wa akaunti za muda mfupi na akiba (CASA) **uliimarika**

**27.5%** in 2024 | ONGEZEKO | **34.2%** in 2025

**HATUA ZA KIMKAKATI ZA KUKUZA NA KUONGEZA AMANA ZA GHARAMA NAFUU**

- Kuongeza amana za gharama nafuu
- Kupunguza kutegemea fedha za gharama
- Kupanua na kutofautisha vyanzo vya fedha

### Muhtasari wa Utendaji

Kwa mwaka wa fedha 2025, benki ilifanikiwa kupunguza hasara yake kabla ya kodi kwa kiwango kikubwa kutoka Tsh bilioni 1.7 mwaka 2024 hadi Tsh milioni 347. Vilevile, hasara baada ya kodi ilipungua kutoka Tsh milioni 969 hadi Tsh milioni 635. Hali hii inaakisi kupungua kwa hasara kabla ya kodi kwa asilimia 80 na baada ya kodi kwa asilimia 34.6, ikithibitisha maendeleo ya benki katika kuimarisha utendaji wake na kujenga ustahimilivu katika mazingira ya biashara yenye ushindani.

Mapato halisi ya riba kabla ya tengo la mikopo chechefu yaliongezeka hadi kufikia Tsh bilioni 15.3 kutoka Tsh bilioni 13.0 mwaka 2024, ongezeko la asimilia 17.7. Hii ilichangizwa na ukuaji wa mikopo na maboresho ya viwango vya riba. Baada ya tengo la mikopo chechefu, mapato halisi ya riba yaliongezeka hadi kufikia Tsh bilioni 13.8 ikilinganishwa na Tsh bilioni 10.9 mwaka 2024, ongezeko la asilimia 26.6. Jumla ya mapato ya kiundeshaji yaliongezeka kutoka Tsh bilioni 17.2 mwaka 2024 hadi Tsh bilioni 19.4, ongezeko la asilimia 12.8 likionyesha uimara wa shughuli za msingi za kibenki. Gharama za uendeshaji zilifikia Tsh bilioni 19.7 kutoka Tsh bilioni 18.9 mwaka 2024, ongezeko la asilimia 4.2. Hii ilichangizwa na shinikizo la mfumuko wa bei na uwekezaji wa kimkakati.

### Utendaji wa Mizania ya benki

Mizania ya benki iliendeleza kuwa imara, ambapo jumla ya mali ziliongezeka hadi kufikia Tsh bilioni 260.8 kutoka Tsh bilioni 259.6 mwaka 2024, ongezeko la asilimia 0.5. Hii ilichangiwa na ukuaji wa mikopo kutoka Tsh bilioni 132.4 mwaka 2024 hadi Tsh bilioni 133.3, ongezeko la 0.7. Amana za wateja zilikua hadi kufikia Tsh bilioni 150. Uwiano wa akaunti za muda mfupi na akiba (CASA) uliimarika kwa kiasi kikubwa kutoka asilimia 27.5 hadi 34.2 ikionyesha maendeleo katika uhamasishaji wa amana za gharama nafuu. Hatua za kimkakati kama LIPA Namba, kampeni za kujisajili wateja kidigitali, ushirikiano wa benki na Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo (SACCOS) na Kampuni za Teknolojia za Kifedha (Fintechs) ziliendelezwa. Mikakati hii ililenga kuongeza amana za gharama nafuu na kupanua wigo wa vyanzo vya fedha, hivyo kuimarisha ufanisi wa shughuli za benki. Hatua hizi zinaunga mkono moja kwa moja dhamira yetu ya muda mrefu ya kupunguza gharama ya uendeshaji. Mtaji wa wanahisa uliimarika kutoka Tsh 30.9 bilioni 2024 hadi Tsh bilioni 33.6, ongezeko la asilimia 8.7.

### Usimamizi wa Mtaji

Benki iliendelea kusimamia mtaji wake, ikilenga kuimarisha akiba na kuboresha mgawanyo wa mali. Kufikia tarehe 31 Disemba 2025, viwango vya mtaji vilikidhi matakwa ya kisheria, ambapo uwiano wa mtaji wa Daraja la kwanza ulikuwa asilimia 15.34 na uwiano wa jumla ya mtaji ulikuwa asilimia 16.31, ukizidi viwango vya chini vya kisheria vilivyowekwa na Benki Kuu vya asilimia 12.5 na asilimia 14.5 mtawalia. Mtaji huu unaonyesha benki iko imara na ina nafasi ya kufanya biashara zaidi ili kuongeza thamani ya wanahisa.



Bertha Munyera
Mkurugenzi wa Fedhae
DCB Commercial Bank Plc





### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA UNAOISHIA 31 DESEMBA 2025

| | Notes | 2025 TZS'000 | 2024 TZS'000 |
|---|---|---|---|
| Mapato ya Riba | 8 | 34,871,887 | 32,277,746 |
| Gharama za Riba | 9 | (19,527,406) | (19,234,099) |
| **Mapato halisi ya Riba** | | **15,344,481** | **13,043,647** |
| Ongezeko la tengo katika mikopo | 23 | (1,579,010) | (800,600) |
| Ongezeko la tengo katika mali nyingine | 23 | (7,416) | (1,304,527) |
| MAPATO HALISI YA RIBA BAADA YA ONGEZEKO LA TENGO KATIKA MIKOPO | | 13,758,055 | 10,938,520 |
| Mapato ya ada na kamisheni | 10 | 3,824,518 | 4,311,805 |
| Mapato ya fedha za kigeni | 11 | 576,656 | 650,739 |
| Mapato mengine | 12 | 1,190,910 | 1,256,464 |
| **Jumla ya mapato yasiyo ya Riba** | | **5,592,084** | **6,219,008** |
| JUMLA YA MAPATO YA KIUNDESHAJI | | **19,350,139** | **17,157,528** |
| GHARAMA ZA UENDESHAJI | | | |
| Gharama za wafanyakazi | 13 | (10,326,361) | (10,123,616) |
| Gharama za ujumla za kiutawala | 14 | (6,722,742) | (5,751,174) |
| Gharama za uchakavu | 15 | (2,647,706) | (2,998,046) |
| JUMLA YA GHARAMA ZA UENDESHAJI | | (19,696,809) | (18,872,836) |
| HASARA KABLA YA MAKATO YA KODI | | (346,670) | (1,715,308) |
| Tengo la kodi ya mapato | 19 | (288,005) | 746,265 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | | (634,675) | (969,043) |
| MAPATO MENGINE KIUJUMLA | | | |
| Thamani ya faida katika uwekezaji | | | |
| Uwekezaji wa Hisa – Ongezeko la thamani katika Uwekezaji | | 162,392 | 974,073 |
| Makato katika mali ya kodi iliyoahirishwa | | | (292,222) |
| Ongezeko la thamani katika uwekezaji | | 162,392 | 681,851 |
| Jumla ya faida/hasara kwa mwaka | | 472,283) | (287,192) |
| Mapato kwa hisa | 34 | (3.31) | (5.95) |

Taarifa za fedha zilizopo kwenye kurasa namba 129 had 211 za kitabu cha taarifa za mahesabu za mwaka 2024, ziliidhinishwa na kusainiwa na Bodi ya Wakurugenzi tarehe 31 Machi, 2026.

## WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 DESEMBA 2025

| | Notes | 2025 TZS'000 | 2024 TZS'000 |
|---|---|---|---|
| **Mali** | | | |
| Fedha Taslim na salio na Benki Kuu ya Tanzania | 20 | 27,380,493 | 20,692,065 |
| Salio katika benki nyingine na taasisi za fedha | 21 | 14,003,758 | 19,388,108 |
| Uwekezaji katika amana za serikali na amana nyingine | 22 | 62,938,400 | 62,049,681 |
| Mikopo na vianzio kwa wateja | 23 | 133,317,973 | 132,406,004 |
| Kodi ya kampuni inayoweza kurejeshwa | 28 | - | 288,005 |
| Mali na vifaa | 25 | 1,905,744 | 2,326,927 |
| Haki ya matumizi ya mali zilizokodiwa | (i)36 | 5,689,831 | 6,058,029 |
| Mali zisizoshikika | 26 | 2,791,171 | 3,027,713 |
| Kodi ya mapato iliyoahirishwa | 30 | 7,507,868 | 7,507,868 |
| Uwekezaji katika amana za hisa | 24 | 3,204,664 | 3,042,273 |
| Mali nyingine | 27 | 2,104,297 | 2,349,636 |
| Jumla ya mali | | 260,844,199 | 259,136,309 |
| | | | |
| **Dhima** | | | |
| Amana kwa benki zingine | a.29 | 39,826,968 | 36,419,080 |
| Amana kutoka kwa wateja | b.29 | 150,526,851 | 152,039,156 |
| Kodi | | 34,127 | |
| Mikopo | 31 | 29,260,167 | 32,738,415 |
| Dhima zingine | 32 | 3,872,138 | 3,096,390 |
| Dhima za ukodishaji | (ii)36 | 3,737,048 | 3,874,347 |
